ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (154-165), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

KUAINISHA FURSA ZA LUGHA YA KISWAHILI ZILIZOPO KWENYE MITAALA MIPYA KATIKA SERA ILIYOBORESHWA NCHINI TANZANIA

Bertha Benitho[1], Dkt. Mussa Omary Amanzi[2]

[1]Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro, Barua pepe; S.L.P 1031 Morogoro Tanzania

[2]Idara ya Kiswahili, Chuo Kikuu cha Waislamu cha Morogoro, Barua pepe; S.L.P 1031, Morogoro, Tanzania S.L.P 1031, Morogoro Tanzania.

DOI: https://doi.org/10.5281/zenodo.23499480

Published Date: 20-October-2026

IKISIRI: **Makala hii imejikita katika kuchunguza fursa za lugha ya Kiswahili zilizopo kwenye mitaala mipya katika Sera mpya wa elimu nchini Tanzania iliyoboreshwa. Kwa kuzingatia mabadiliko ya sera mpya ya elimu, Makala haya yamechunguza kwa kina namna Vyuo Vikuu vinavyobuni na kutekeleza mipango ya kimkakati ya kukuza Kiswahili katika mazingira ya kisasa ya elimu. Utafiti huu ulihusisha wataalamu kutoka Vyuo Vikuu vinne. Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) , Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), Chuo kikuu cha Waislamu cha Morogoro (MUM) na Chuo Kikuu Mzumbe(MU). Utafiti ulitumia usampulishaji lengwa kwa kuchagua (wakuu wa idara) na usampulishaji lengwa mpokezano (kwa wahadhiri) kutoka taasisi nne: , kila chuo kikiwa na washiriki watano. Data kutoka kwa wataalamu wa Kiswahili zilikusanywa kwa usaili wa ana kwa ana na uchambuzi wa nyaraka. Uchambuzi wa data ulitumia mkabala wa kimaelezo ili kupata taswira pana na sahihi. Utafiti umeongozwa na Nadharia ya Uamilifu ya Emile Durkheim, inayosisitiza umuhimu wa lugha kama kiungo cha mshikamano wa kijamii na maendeleo ya kitaifa. Matokeo yanaonesha kuwa taasisi za Kiswahili zina mikakati ya kuendeleza lugha hii kwa kuzingatia mabadiliko ya mitaala na matumizi ya TEHAMA, ingawa utekelezaji wake unakabiliwa na changamoto za rasilimali, ushirikiano na ufuatiliaji. Utafiti huu unatoa mwelekeo mpya wa kitaalamu kwa kubainisha nafasi ya Kiswahili katika elimu, biashara na utawala, huku ukitoa mapendekezo ya kisera yatakayowezesha matumizi bora na endelevu ya lugha hii katika maendeleo ya taifa.**

Maneno Muhimu; **Sera ya Elimu na Mafunzo, Kiswahili, Mitaala, Vyuo Vikuu, Uamilifu wa Kijamii, TEHAMA.**

1. UTANGULIZI

Lugha ni nyenzo muhimu katika mawasiliano, upatikanaji

wa maarifa na maendeleo ya jamii. Nchini Tanzania, Kiswahili kina nafasi ya pekee kama lugha ya Taifa inayotumika katika mawasiliano, elimu na kuendeleza utamaduni wa Watanzania. Kutokana na umuhimu huo, maboresho ya sera na mitaala ya elimu yanaweza kutoa fursa mbalimbali za kukuza na kupanua matumizi ya lugha hii katika nyanja tofauti za maisha.

Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, (Toleo la 2023) ,imeweka mkazo katika kuimarisha matumizi ya lugha katika mawasiliano na elimu. Sera hiyo inasisitiza matumizi ya Kiswahili katika elimu ya awali na msingi, huku ikitambua nafasi ya lugha nyingine katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo (Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, 2023). Aidha, mitaala iliyoboreshwa inalenga kujenga umahiri unaowawezesha wanafunzi kutumia maarifa na ujuzi katika mazingira halisi ya maisha. Ministry of Education Tanzania.

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (154-165), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

Katika mazingira hayo, ni muhimu kuchunguza fursa zinazoweza kujitokeza kwa lugha ya Kiswahili kupitia mitaala mipya. Fursa hizo zinaweza kujumuisha ajira katika ufundishaji, uandishi wa vitabu, tafsiri, uhariri, utafiti wa lugha na uandaaji wa zana za kidijitali za kujifunzia. Hivyo, makala hii inalenga kuainisha fursa za lugha ya Kiswahili zilizopo katika mitaala mipya kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo iliyoboreshwa nchini Tanzania. Aidha, makala inalenga kuonesha umuhimu wa kuzitambua na kuzitumia fursa hizo katika kukuza lugha ya Kiswahili na kuongeza mchango wake katika maendeleo ya Taifa.

Mwelekeo mpya wa elimu katika Sera ya mwaka 2014 toleo la mwaka 2023 umetolana na kuchakata maoni ya wadau. Pia umetokana na kurejelea falsafa ya elimu ya kujitegemea ya mwaka 1967; Sheria ya elimu Na.25 ya mwaka 1978 na Sera ya Elimu ya mafunzo ya mwaka 1995. Vilevile, kiunzi cha Taifa cha mitaala wa elimumsingi na elimu ya ualimu cha mwaka 2019 na ripoti ya mapendekezo ya elimu nchini Tanzania (Tume ya makweta) ya mwaka 1982. Aidha, mwelekeo mpya wa elimu ulozingatia mahitajio ya kijamii na kiuchumi ya sasa na kupitia matamko ya kisera ya na kisheria ya kitaifa, kikanda na kimataifa. Mwelekeo mpya wa elimu nchini Tanzania umetokana pia na machapisho yanayoonesha mifumo ya elimu ya nchi mbalimbali ikiwemo Zambia, Mauritius, Ghana, Kenya, Ufini, Singapore,Ureno, Ujerumani China na Malaysia ili kupata uzoefu wao.(Sera ya Elimu, 2014 toleo la mwaka 2023)

Kabla ya mwelekeo huu mpya wa elimu, bado lugha ya Kiswahili ilitambulika kuwa lugha ya Taifa lakini pia ni lugha inayotumika kufundishia na kujifunzia katika shule za msingi. Somo la Kiswahili ni somo la lazima katika elimu ya sekondari ya chini. Aidha wataalamu mbalimbali wamefanya tafiti kadhaa zilizosaidia katika kutathmini matumizi ya fursa hizo (taz.kwa mfano Gibbe,1983, Mazrui na Shariff 1994; Mazrui na Alamin, 1998, Massamba, (2007), Maganga, 2008; Matei, 2008, Mutembei, 2011; Odeo na wamalwa, (2017) na Adolph, (2023) Kwa ujumla tafiti za wataalamu hawa ziliongeza chachu katika utumizi wa fursa za lugha ya Kiswahili zilikuwapo.

Katika mwelekeo huu mpya wa elimu nchini Tanzania, fursa za lugha ya Kiswahili zimeongezejka sana. Fursa zilizoongezeka katika mwelekeo huu ni pamoja ufundishaji wa somo la Kiswahili umeegemea kwenye mawasiliano zaidi na sio uchambuzi pekee. Pia lugha ya Kiswahili inafundishwa kama bidhaa ambapo umahiri kama vile; tafsiri, ukalimani, utungaji na uandishi, ufundishaji wa Kiswahili kwa wageni, uchapaji na uchapishaji nk.umesisitozwa Kwa kupewa kipaumbele sana katika mwelekeo huu mpya. Ulinganishi wa lugha ya Kiswahili na lugha na lugha nyingine ni kama fursa nyingine iliyopo kwenye mwelekeo huu mpya. Mitaala ya lugha zote imepangwa Kwa mtindo mmoja, Kwa hiyo ni rahisi mno Kwa anayejifunza Kiswahili kujifunza lugha nyingine.Masomo ya ufundi ambayyo yameingizwa katika mitaala elimu wa secondari yamepangwa kufundishwa Kwa lugha ya Kiswahili. SI hivyo tu mitaala mpya katika mwelekeo huu mpya wa elimu katika kiwango cha sekondari unaruhusu kuwa na shule ambazo zitafundisha masomo yote kwa kutumia lugha ya Kiswahili kasoro masomo ya lugha za kigeni tu (taz. mitaala mpya wa elimu wa mwaka 2023)

Kama ilivyokuwa kwenye mielekeo ya elimu kabla ya mwelekeo huu mpya, tafiti, mbalimbali zilifanyika kuchochea utumizi wa fursa za lugha ya Kiswahili za wakati huo, basi ipo haja ya kuwa na tafiti mpya zinachunguza na kuchochea utumizi wa fursa za lugha ya Kiswahili za wakati huo basi, ipo haja ya kuwa na tafiti mpya zinachunguza na kuchochea utumizi wa fursa hizo mpya zinazoongezeka. Kwa uelewa wa mtafiti kupitia maandiko mbalimbali, hakuna tafiti mpya zinazochunguza na kuchochea utumizi wa fursa hizi mpya katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, makala haya yamekusudia kuchunguza fursa za lugha katika matumizi ya fursa za lugha kwenye mielekeo mpya wa elimu nchini Tanzania

2. KIUNZI CHA NADHARIA

Makala hii iliongozwa na Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii iliyoasisiwa na Émile Durkheim (1858-1917) na baadaye kuendelezwa na Talcott Parsons (1937) na Robert K. Merton (1949) Nadharia hii hueleza kuwa jamii ni mfumo unaoundwa na taasisi zinazotegemeana, ambapo kila taasisi hutekeleza kazi maalumu katika kudumisha utulivu, mshikamano na maendeleo ya jamii. Kwa mtazamo huu, mfumo wa elimu ni mojawapo ya taasisi muhimu zinazohusika na utoaji wa maarifa, ujuzi, maadili na rasilimali watu zinazohitajika katika maendeleo ya taifa. Hivyo, mabadiliko ya sera za elimu huzilazimu taasisi za elimu kufanya maboresho ya mitaala, mbinu za ufundishaji na programu za kitaaluma ili kuendana na mahitaji mapya ya jamii (Durkheim, 1984).

Kwa mujibu wa nadharia hii, ustawi wa mfumo wa elimu hupimwa kwa uwezo wake wa kuitikia mahitaji ya jamii kupitia utoaji wa wahitimu wenye maarifa na ujuzi unaofaa mazingira ya kijamii, kiuchumi na kiteknolojia yanayobadilika. Katika mantiki ya makala hii, maboresho ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Toleo la 2023) yanatazamwa kama mabadiliko ya kimfumo yanayozitaka taasisi za elimu ya juu kurekebisha mitaala ya Kiswahili ili kuandaa

wataalamu wanaoweza kutosheleza mahitaji mapya ya elimu, soko la ajira na maendeleo ya taifa. Kwa hiyo, vyuo vikuu vinatarajiwa kuboresha programu za kitaaluma, kuanzisha kozi mpya na kutumia mbinu bunifu za ufundishaji ili kuongeza mchango wa Kiswahili katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ilifaa kuongoza utafiti huu kwa kuwa ilitoa msingi wa kuchunguza namna vyuo vikuu vinavyoitikia maboresho ya sera kupitia mipango ya kuboresha mitaala ya Kiswahili. Iliwezesha kutathmini uhusiano kati ya sera ya elimu, mipango ya taasisi na mahitaji ya jamii kwa kuzingatia kwamba mabadiliko katika sera yanapaswa kuakisiwa katika utekelezaji wa mitaala na maandalizi ya wahitimu. Aidha, nadharia hii ilisaidia kufafanua mchango wa programu mpya za Kiswahili, matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), pamoja na taaluma za tafsiri, ukalimani, uhariri na uandishi katika kuimarisha nafasi ya Kiswahili kama rasilimali ya maendeleo.

Hata hivyo, nadharia hii imesahihishwa kwa kuzingatia zaidi utulivu na mshikamano wa jamii kuliko migongano, tofauti za kimasilahi na changamoto zinazoweza kujitokeza katika utekelezaji wa sera za elimu. Pamoja na ukomo huo, ilifaa kwa makala hiikua kwa kuwa lengo kuu lilikuwa kuainisha fursa tza lugha ya Kiswahili zilizopo kwenye mitaala mipya katika sera iliyoboreshwa badala ya kuchunguza migongano ya kisera au kisiasa. Kwa msingi huo, Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ilitoa mwongozo unaofaa katika uchambuzi na ufasiri wa matokeo ya uchunguzi.

3. METHODOLOJIA

Makala haya yalitumia mkabala wa ubora kwa kuwa ulilenga kupokea kuainisha uelewa kuhusu namna vyuo vikuu vinavyoboresha mitaala ya Kiswahili kufuatia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Toleo la 2023). Mkabala huu ulifaa kwa sababu uliwezesha kuchunguza mitazamo, uzoefu na mikakati inayotekelezwa na wataalamu wa Kiswahili katika taasisi za elimu ya juu. Utafiti ulifuata muundo wa kimaelezo uliowezesha kueleza na kuainisha fursa za lugha ya Kiswahili zilizopo kwenye mitaala mipya katika sera iliyoboreshwa nchini Tanzania.

Utafiti ulifanyika katika Vyuo Vikuu vitatu vinavyotoa programu za Kiswahili, ambavyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Chuo A), Chuo Kikuu cha Dodoma (Chuo B), na Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (Chuo C). Vyuo hivi vilichaguliwa kwa makusudi kutokana na uzoefu wake katika ufundishaji wa Kiswahili na ushiriki wake katika maboresho ya mitaala yanayohusiana na sera mpya ya elimu.

Washiriki wa makala walikuwa wataalamu 20 wa Kiswahili, wakiwemo wakuu wa idara wanne na wahadhiri 16. Wakuu wa idara walipatikana kwa kutumia usampulishaji lengwa kutokana na nafasi yao katika usimamizi wa programu za Kiswahili, huku wahadhiri wakipatikana kwa usampulishaji wa mpokezano kwa kuzingatia uzoefu wao katika maendeleo ya mitaala na utekelezaji wa programu za kitaaluma.

Data zilikusanywa kwa kutumia usaili wa ana kwa ana na uchambuzi wa nyaraka. Usaili uliwezesha kupata taarifa kuhusu aina za fursa zilizopo kwenye mitaala mipya katika sera iliyoboreshwa, utekelezaji wa maboresho ya mitaala, changamoto zilizojitokeza na mikakati ya kuimarisha Kiswahili katika elimu ya juu. Uchambuzi wa nyaraka ulihusisha kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Toleo la 2023), mitaala ya Kiswahili ya vyuo husika, mihtasari ya kozi, pamoja na nyaraka nyingine za kitaasisi ili kuthibitisha taarifa zilizopatikana kupitia usaili.

Data zilichambuliwa kwa kutumia uchambuzi wa maudhui kwa kuzipanga katika mada kuu zilizoibuliwa kutokana na malengo ya utafiti. Uchambuzi uliongozwa na Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ili kufafanua uhusiano kati ya maboresho ya sera, aina za fursa na mahitaji ya jamii. Ili kuimarisha uaminifu wa matokeo, taarifa zilizopatikana kupitia usaili zililinganishwa na ushahidi kutoka katika nyaraka rasmi (triangulation). Aidha, utafiti ulizingatia maadili ya utafiti kwa kupata ridhaa ya washiriki, kulinda usiri wa taarifa zao na kuhakikisha kuwa ushiriki wao ulikuwa wa hiari katika hatua zote za utafiti.

4. MATOKEO NA MJADALA

Sehemu hii inawasilisha uchambuzi wa fursa za kiuchumi na kitaaluma zinazotokana na lugha ya Kiswahili zilizomo kwenye mitaala mipya ya elimu kufuatia maboresho ya sera ya elimu ya mwaka 2023 nchini Tanzania. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya usomaji wa machapisho, ambapo mtafiti alichambua machapisho mbalimbali yanayohusiana na lengo la kwanza, ikiwemo: sera mpya ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Toleo la 2023), mtaala wa Elimu ya sekondari kidato cha I-IV (2023), Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI (2023), Muhtasari wa Kiswahili Elimu ya Sekondari: Kidato cha I-IV, na Muhtasari wa Kiswahili Elimu ya Sekondari: Kidato cha V-VI (2023).

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (154-165), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

Makala haya yamebaini kuwepo kwa fursa nane za kiuchumi na kitaaluma zinazojitokeza katika Sera na Mtaala Mpya wa Elimu nchini Tanzania. Fursa hizo zinahusiana na kujiajiri, kupata kipato na kuendeleza taaluma kupitia Kiswahili, nazo ni: tafsiri na ukalimani, uandishi na uhariri, ubunifu wa kilugha, ubidhaishaji wa lugha, sanaa na uigizaji, Kiswahili kama Lugha ya Kufundishia, na matumizi ya TEHAMA na Ubunifu katika Ufundi wa Lugha. Fursa hizi zimeelezwa kama ifuatavyo:

4.1 Fursa za Tafsiri na Ukalimani

Kwa mujibu wa Mshindo (2010), tafsiri ni kufafanua maana ya matini moja na kutayarisha baadae matini nyingine inayowiana nayo ambayo huitwa tafsiri na ambayo inawakilisha ujumbe uleule uliomo katika matini ya awali kwa kutumia lugha nyingine. Kwa mujibu wa TATAKI (2019), ukalimani ni uhawalishaji wa taarifa au ujumbe kutoka kwa msemaji wa lugha chanzi kwenda katika lugha lengwa kawa njia ya mdomo au mazingumzo. Kwa ujumla, tafsiri ni ujuzi wa kuelewa na kutafsiri maandiko kwa usahihi, wakati ukalimani ni uwezo wa kutafsiri mazungumzo ya mdomo papo kwa papo bila kupoteza maana. Uchambuzi wa Mtaala wa Sekondari wa 2023 unaonesha wazi mwelekeo wa kukuza stadi za lugha na mawasiliano, hususan katika tafsiri na ukalimani.

Tafsiri na ukalimani ni fursa kwa maisha ya mwanafunzi na jamii kwa kuwa hutoa uwezo wa kupata ajira, kujiajiri, na kushirikiana katika nyanja mbalimbali za kazi, ikiwa ni pamoja na utafsiri wa kitaalamu, ukalimani wa biashara na utawala, ufundishaji, vyombo vya habari, huduma za kidijitali, na taaluma za kimataifa. Hivyo, ufahamu na umahiri katika tafsiri na ukalimani unapanua nafasi za ajira, unaongeza thamani yoa kitaaluma na unachangia maendeleo ya kiuchumi. Data za hoja hii zimewasilishwa katika Jedwali Na. 2 na 3:

Jedwali Na. 1: Umahiri wa Tafsiri na Ukalimani (Kidato cha I-IV)

Somo	Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
Kiswahili	Kutafsiri na kukalimani kazi mbalimbali	Kutafsiri matini mbalimbali Kukalimani mazungumzo mbalimbali Kutathmini kazi mbalimbali za tafsiri Kutathmini ukalimani

Chanzo: Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV (2023, uk. 10)

Jedwali Na. 2 linaonesha umahiri unaotakiwa katika somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa Kidato cha I hadi IV, likilenga kutafsiri na kukalimani kazi mbalimbali. Umahiri huu unajumuisha kutafsiri matini, kukalimani mazungumzo, na kutathmini kazi za tafsiri na ukalimani ili kuhakikisha ujumbe unaeleweka ipasavyo. Jedwali Na. 3 linaonesha umahiri huu huu kwa kidato cha V na VI.

Jedwali Na. 2: Umahiri wa Tafsiri na Ukalimani (Kidato cha V-VI)

Somo	Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
Kiswahili	Kutoa huduma ya lugha ya Kiswahili katika jamii	Kufanya tafsiri sahili katika lugha ya Kiswahili Kuhariri matini mbalimbali za Kiswahili Kufanya ukalimani sahili kwa lugha ya Kiswahili

Chanzo: Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V - VI (2023, uk. 24)

Data za Jedwali Na. 2 na 3 zinaonesha kuwa mtaala wa Kiswahili katika sekondari unalenga kuendeleza umahiri wa tafsiri na ukalimani kwa wanafunzi katika ngazi zote za elimu ya sekondari. Kwa Kidato cha I-IV (Jedwali 2), umahiri unahusisha kutafsiri matini mbalimbali, kukalimani mazungumzo, na kutathmini kazi za tafsiri na ukalimani, ili kuhakikisha wanafunzi wanaweza kuelewa na kuwasilisha ujumbe ipasavyo. Kwa Kidato cha V-VI (Jedwali 3), umahiri unalenga zaidi kwenye kutoa huduma ya lugha ya Kiswahili katika jamii, ikiwemo kutafsiri na kukalimani kwa ufasaha na kuhariri matini mbalimbali, jambo linalolenga kuongeza uwezo wa wanafunzi kutumia Kiswahili kikamilifu katika mazingira halisi ya kijamii.

Kulingana na Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ya Émile Durkheim, jamii hudumisha utulivu na maendeleo yake kupitia taasisi mbalimbali zinazotekeleza majukumu maalumu kwa manufaa ya jamii nzima. Miongoni mwa taasisi hizo, elimu

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (154-165), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

ina nafasi muhimu ya kuendeleza maadili, maarifa, na stadi zinazohitajika ili kuimarisha mshikamano na utendaji wa kijamii. Kwa mujibu wa nadharia hii, elimu si chombo cha kukuza maendeleo ya mtu binafsi pekee, bali pia ni nyenzo ya kuwaandaa wanajamii kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii na kiuchumi. Katika muktadha huu, mtaala wa Kiswahili huandaa wanafunzi kuwa wataalamu wa tafsiri, ukalimani, uhariri na huduma nyingine za lugha zinazohitajika katika jamii. Hivyo, mtaala huu huchangia maendeleo ya wahitimu binafsi sambamba na kuimarisha mawasiliano, utoaji wa huduma za lugha, na mshikamano wa kijamii. Kwa mtazamo wa Durkheim, mchango huu unaifanya elimu ya Kiswahili kuwa sehemu muhimu ya mfumo wa kijamii kwa kuzalisha wataalamu wanaokidhi mahitaji ya jamii na kuendeleza ufanisi wa kijamii.

Data hizi za mtaala wa Kiswahili wa sekondari wa 2023 zinatoa fursa muhimu kwa Vyuo Vikuu vinavyofundisha Kiswahili, kwani zinatengeneza msingi imara wa ujuzi wa tafsiri na ukalimani unaohitajika katika huduma za kitaaluma na kijamii. Kwa kuzingatia mtaala, umahiri wa wanafunzi katika kutafsiri, kukalimani, na kuhariri maandiko ya Kiswahili unawaandaa kuwa wataalamu wa lugha, wenye uwezo wa kutoa huduma za kitaaluma na kuchangia maendeleo ya jamii na sekta mbalimbali. Hii ni fursa kwa Vyuo Vikuu kwa sababu inaweza kurahisisha uanzishwaji wa kozi za taaluma za Kiswahili, kuimarisha utafiti wa lugha, na kukuza ubunifu wa kielimu na kiutamaduni. Hata hivyo, changamoto hujitokeza pale panapokosekana vifaa vya kutosha, mafunzo ya kisasa ya ukalimani na tafsiri, na mtaala unaoendana na mahitaji ya soko la kazi; bila haya, fursa ya kuendeleza ujuzi huu kikamilifu inaweza kushindikana. Hata hivyo, fursa hii inachangia mshikamano wa kijamii kwa kuwa wanafunzi walio na ujuzi huu wanakuwa watumishi wa lugha wanaosaidia kuimarisha mawasiliano, utulivu, na maendeleo ya jamii kwa ujumla.

4.2 Fursa za Uandishi na Uhariri

Kwa mujibu wa TATAKI (2019), uandishi ni neno litokanalo na kitenzi “andika” ambacho maana yake ni mchakato wa kuunda maandiko ili kuwasilisha mawazo, taarifa, au ujumbe kwa uwazi na ufasaha, jambo linalowezesha mawasiliano bora na kueleweka kwa wote wanaohusika. Uhariri ni mchakato wa kusoma, kukagua na kusahihisha (kuboresha) miswada ili kuhakikisha usahihi wa lugha, mtindo na uelewa kwa wasomaji (TATAKI, 2019). Uandishi na uhariri ni fursa kwa wanafunzi na wahitimu wa Kiswahili kwani vinawawezesha kujiajiri, kupata kipato, na kutoa huduma za kitaalamu katika elimu, utawala, vyombo vya habari, biashara, TEHAMA, na sanaa, hivyo kuchangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Data zilizokusanywa kutoka kwenye Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I - IV (2023) na Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V - VI (2023) zimechambuliwa na kuwasilishwa katika Jedwali Na. 4 na 5, zikionesha umahiri unaohitajika katika uandishi na uhariri wa Kiswahili kwa wanafunzi wa sekondari. Jedwali Na. 4 linaonesha ushahidi huu.

Jedwali Na. 3: Umahiri wa Uandishi (Kidato cha I-IV)

Somo	Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
Kiswahili	Kuwasiliana katika miktadha mbalimbali	Kuwasiliana kwa njia ya maandishi katika miktadha mbalimbali

Chanzo: Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha I-IV (2023, uk. 23)

Jedwali Na. 4 linaonesha kipengele cha “Umahiri wa Uandishi na Uhariri” kwa somo la Kiswahili katika ngazi ya Kidato cha I–IV. Nalo Jedwali Na. 5 linawasilisha data ya uhariri kama ilivyobainika katika Mtaala wa Elimu ya Sekondari (2023).

Jedwali Na. 4: Umahiri wa Uhariri (Kidato cha V-VI)

Somo	Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
Kiswahili	Kuhariri kazi mbalimbali	Kumudu stadi za uhariri

Chanzo: Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI (2023, uk. 10)

Data za Jedwali Na. 4 na 5 zinaonesha kuwa mtaala wa Kiswahili katika sekondari unalenga kuendeleza ujuzi wa wanafunzi katika kuandika, kuboresha na kutafsiri maandiko. Kwa Kidato cha V-VI, mwelekeo unahusiana zaidi na matumizi ya lugha katika jamii, ikiwemo tafsiri sahili, uhariri, na ukalimani. Data hizi zinatoa fursa kwa wanafunzi kujenga ujuzi wa kiutendaji unaoweza kutumika si tu darasani bali pia katika maisha ya kijamii na kitaalamu, huku

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (154-165), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

zikichangia kuimarisha mawasiliano na huduma za lugha, jambo linaloongeza thamani ya Kiswahili kama lugha ya mawasiliano na huduma.

Hoja hii inaendana moja kwa moja na Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ya Émile Durkheim, kwa kuwa inadhihirisha jinsi elimu ya uandishi na uhariri inavyotekeleza jukumu muhimu katika kudumisha mshikamano na utendaji wa kijamii. Kwa mujibu wa Durkheim, kila kipengele cha jamii kina kazi maalumu ya kuchangia katika uthabiti na maendeleo ya jamii. Hivyo, uandishi na uhariri katika mtaala wa Kiswahili hufanya kazi ya kijamii kwa kuimarisha mawasiliano, uwazi wa taarifa, na usambazaji wa maarifa, misingi muhimu ya mshikamano wa kijamii.

Kulingana na uchambuzi wa mtafiti, mafunzo ya uandishi na uhariri katika mtaala wa Kiswahili husaidia wanafunzi kuendeleza ujuzi wa kitaalamu unaoweza kutumika katika nyanja mbalimbali kama elimu, utawala, vyombo vya habari, na taasisi za kimataifa. Hii ni fursa kwa sababu inawawezesha wanafunzi kujenga taaluma yenye thamani, kupata ajira, na kuchangia katika ustawi wa kijamii na kiuchumi. Aidha, uandishi na uhariri husaidia jamii kufanya kazi kwa ufanisi, kwa kuimarisha mawasiliano sahihi, usambazaji wa taarifa, na ushirikiano, jambo linaloongeza mshikamano wa kijamii na maendeleo ya taifa.

Kwa Vyuo Vikuu vinavyofundisha Kiswahili, hii ni fursa kwa sababu mtaala unazalisha hitaji la wataalamu wenye ujuzi wa uandishi wa Kiswahili, ikiwa ni pamoja na walimu, waandishi, wahariri, na wataalamu wa TEHAMA. Hii inawawezesha vyuo kuongeza idadi ya taaluma, kukuza ajira kwa wahitimu, kuchangia ukuaji wa taaluma na uchumi wa ubunifu, kuhifadhi maarifa ya kitaifa, na kuendeleza ujuzi wa kiutendaji wa wanafunzi unaotumika katika sekta mbalimbali za kijamii na kiutawala. Hii inaashiria kwamba Kiswahili kama taaluma ina nguvu ya kuimarisha mshikamano wa kijamii na kukuza maendeleo ya kitaifa kupitia elimu, uandishi, na huduma za lugha. Hata hivyo, changamoto zipo, zikiwemo ukosefu wa vifaa vya kisasa vya kufundishia, upungufu wa wataalamu waliobobea katika teknolojia ya lugha, na mitazamo hasi ya kijamii kuhusu thamani ya Kiswahili katika soko la ajira, mambo ambayo yanahitaji mikakati madhubuti ya kitaasisi na kitaifa ili kukabiliana nayo.

4.3 Fursa za Sanaa na Uigizaji

Kwa mujibu wa Matundura (2007), sanaa ni uwezo wa kuonesha ubunifu wa kibinadamu kupitia uandishi, muziki, uchoraji, uigizaji na maonyesho mbalimbali ili kufikisha ujumbe kwa njia ya kuvutia. Uigizaji, kama kipengele muhimu cha sanaa, inahusisha fani ya kuigiza au kuonyesha tabia, hisia na matukio kwa njia ya maonyesho (Malaga, 2021). Sanaa na uigizaji ni fursa kwa kipato na ajira kwa kuwa vinatoa nafasi kwa watu kujihusisha na kazi za ubunifu kama uandishi wa tamthilia, uigizaji, utayarishaji wa filamu, muziki, na matangazo ya redio na televisheni. Kupitia vipaji hivi, wasanii wanaweza kujiajiri, kupata kipato, na kukuza ajira katika sekta ya burudani na utamaduni, hivyo kuendeleza matumizi ya Kiswahili na kuchangia maendeleo ya kiuchumi. Hoja hii imetolewa kwenye Mtaala wa Elimu ya Sekondari (Kidato cha I-VI, 2023), kama ilivyobainishwa katika Jedwali Na. 6.

Jedwali Na. 5: Umahiri wa Sanaa na Uigizaji (Kidato cha V-VI)

Somo	Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
Sanaa za Maonyesho	Kukuza uelewa wa dhana, nadharia na kanuni za Sanaa za Maonyesho	1 Kuelezea maendeleo ya sanaa za maonyesho na matapo yake
		2 Kuelezea historia na kanuni za uandishi, uigizaji na uongozaji wa kazi za sanaa za maonyesho
		3 Kumudu mbinu na kanuni za kubaini maeneo ya kufanyia sanaa za maonyesho
		4 Kumudu kanuni za kusimamia matamasha ya sanaa za maonyesho
	Kufanya sanaa za maonyesho	1 Kubuni kazi za sanaa za maonyesho kwa ajili ya jukwaa, filamu, redio na televisheni
		2 Kuigiza na kuongoza kazi za sanaa za maonyesho za jukwaani, filamu, redio na televisheni
		3 Kutumia TEHAMA katika sanaa za maonyesho
		4 Kuonesha uelewa wa misingi na kanuni za maadili katika sanaa za maonyesho

Chanzo: Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V - VI (2023, uk. 27)

Jedwali Na. 6 linaonesha kuwa umahiri wa uandishi na uhariri katika Sanaa za Maonyesho unahusisha uelewa wa nadharia, kanuni, historia na stadi za kiutendaji kama kubuni, kuigiza, kuongoza, na kutumia TEHAMA kwa kuzingatia maadili. Mtaala unalenga kuunganisha maarifa ya nadharia na stadi za vitendo ili kuendeleza umahiri wa kina katika uandishi na uhariri wa sanaa za maonyesho. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ya Émile Durkheim, kila kipengele cha jamii kina mchango katika kudumisha utulivu, mshikamano, na maendeleo ya kijamii. Sanaa na uigizaji, kupitia Kiswahili, huchangia kuimarisha maadili, kukuza umoja wa kitaifa, kutunza utambulisho wa kitamaduni, na kuhifadhi urithi wa taifa, huku pia zikichangia maendeleo ya jamii kwa kutoa fursa za elimu, burudani, ajira, na ukuaji wa kiuchumi. Hivyo, Kiswahili katika sanaa huchukua jukumu la kijamii la kuunganisha watu kupitia ubunifu, burudani, mawasiliano ya kijamii, na mchango wa moja kwa moja katika maendeleo ya jamii.

Sanaa na Uigizaji kupitia Kiswahili ni fursa muhimu kwa Vyuo Vikuu vinavyofundisha Kiswahili. Mtaala wa Kidato cha V-VI unaonesha kuwa wanafunzi wanapopata umahiri wa nadharia na vitendo katika uandishi, uigizaji, na maonyesho, wanajifunza si tu stadi za kiutendaji bali pia kujenga utambulisho wa kitamaduni, kuhifadhi urithi wa taifa, na kukuza umoja wa kitaifa. Hata hivyo, changamoto inaweza kuonekana pale Vyuo Vikuu vinapokosa rasilimali za kutosha, miundombinu ya TEHAMA, au walimu wenye stadi za kina katika sanaa za maonyesho, jambo linaloweza kupunguza ufanisi wa kutumia fursa hii kikamilifu. Kwa hivyo, fursa ipo kwa Vyuo Vikuu, lakini inahitaji uwekaji wa rasilimali na mikakati madhubuti ili kuimarisha umahiri wa Kiswahili katika sanaa na uigizaji.

4.4 Fursa za Ubunifu wa Kilugha

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (2019), ubunifu ni uwezo wa mtu kuanzisha au kuvumbua kitu chochote kipya, chenye utofauti na ubora zaidi, ambacho kina thamani au kinaongeza thamani ya kitu kilichopo, kwa manufaa ya mtu mwenyewe, wateja, na jamii kwa ujumla. Matundura (2007) anafasili ubunifu wa lugha kama matumizi ya lugha kwa njia ya kisanaa na ya kipekee ili kuelezea mawazo, hisia na tajriba za binadamu kwa ubunifu. Kupitia uandishi wa kubuni kama mashairi, tamthilia, na riwaya, lugha hubadilika kuwa chombo cha sanaa kinachoelimisha, kuburudisha, kuhamasisha jamii na kuleta fursa za ajira na kipato. Ubunifu huu unakuwa fursa kwa sababu unawawezesha wanafunzi na watumiaji wa lugha kupata kipato, kujiajiri, na kuunda bidhaa zinazoweza kutumika katika masoko ya elimu, burudani, utawala, biashara, na teknolojia. Kwa mfano, kutunga mashairi, filamu, michezo ya kuigiza, matangazo, programu za kidijitali, na michezo ya kompyuta yenye maudhui ya Kiswahili ni njia za ubunifu zinazoweza kuwa chanzo cha kipato na fursa za ajira.

Kulingana na Mtaala wa Sekondari (Kidato cha I-VI, 2023), ubunifu unachukuliwa kuwa fursa katika Kiswahili kwa sababu unawawezesha wanafunzi na watumiaji kuendeleza mawasiliano, kuunda fasihi na sanaa mpya, na kushiriki katika nyanja za kitaaluma na kiuchumi. Mtaala huu unahusisha masomo ya Sanaa, Muziki, Fasihi, TEHAMA, na Sanaa za Maonyesho, yote yakitoa nafasi ya ubunifu wa kilugha. Hoja kuu ni kwamba Kiswahili kinaweza kuendelezwa kuwa lugha hai ya ubunifu na fursa, ambapo wanafunzi wanahamasishwa kutumia lugha katika kuunda bidhaa zenye thamani, kupata kipato, na kujiendeleza kielimu na kibiashara. Mitaala inabainisha umahiri kama ifuatavyo:

"Kukuza ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano, mawasiliano na mtazamo chanya katika maendeleo yake binafsi na ya taifa" (Mtaala wa Sekondari, Kidato cha I-IV, 2023, uk. 3), na

"Mtaala umejikita katika ujenzi wa umahiri wa msingi katika Stadi za Karne ya 21 ambazo ni kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi..." (Mtaala wa Sekondari Kidato cha V-VI, 2023, uk. 1).

Data inaonesha kuwa mtaala wa Kiswahili unalenga kukuza ubunifu wa kilugha kwa wanafunzi kwa kuzingatia mahitaji ya elimu na maendeleo ya jamii. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ya Émile Durkheim, kila taasisi na shughuli ya kijamii huwa na jukumu maalumu katika kudumisha mshikamano, utulivu na maendeleo ya jamii. Katika muktadha huu, ubunifu wa kilugha unaonekana kama nyenzo muhimu ya kuimarisha mawasiliano, ushirikiano na usambazaji wa maarifa katika jamii. Mtaala unahamasisha matumizi ya Kiswahili kwa njia bunifu katika nyanja mbalimbali kama Sanaa, Fasihi, Muziki, TEHAMA na Sanaa za Maonyesho, ambapo wanafunzi hujengewa uwezo wa kubuni mashairi, tamthilia, filamu, matangazo, maudhui ya kidijitali na kazi nyingine za ubunifu. Kupitia shughuli hizi, wanafunzi hupata stadi muhimu za Karne ya 21 kama fikra tunduizi, uvumbuzi, mawasiliano na ushirikiano, ambazo zinawawezesha kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Kwa mtazamo wa Durkheim, ubunifu wa kilugha unaofundishwa kupitia mtaala wa Kiswahili ni sehemu ya mifumo ya kijamii inayochangia ustawi wa jamii kwa kuandaa wahitimu wenye uwezo wa kutumia lugha kama chombo cha maendeleo, mshikamano wa kijamii na maendeleo endelevu.

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (154-165), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

Ubunifu wa kilugha katika Kiswahili ni dhahiri fursa kubwa kwa Vyuo Vikuu vinavyofundisha Kiswahili. Ubunifu wa lugha kupitia Sanaa, Fasihi, Muziki, TEHAMA, na Sanaa za Maonyesho unakuza stadi za Karne ya 21 na mshikamano wa kijamii, lakini utekelezaji wake unaweza kuzuiliwa na uhakika wa rasilimali na ujuzi wa walimu katika vyuo vinavyofundisha Kiswahili. Hivyo, fursa ipo, lakini utekelezaji wake unahitaji kuungwa mkono kwa rasilimali, mafunzo na sera madhubuti ili kuhakikisha ubunifu huu unakuwa na tija kwa wanafunzi na jamii kwa ujumla

4.5 Fursa za Ubidhaishaji wa Lugha ya Kiswahili

Kwa mujibu wa Mlaga (2021), ubidhaishaji wa lugha ni kutumia lugha kama kitegauchumi cha kupata ajira na kuingiza kipato kupitia burudani, mitandao ya kijamii, michezo, au njia za kisanaa. Ubidhaishaji wa lugha unachukuliwa kuwa fursa kwa sababu unawawezesha watu kutumia ujuzi wa lugha kupata ajira na kuongeza kipato. Hii inaweza kufanyika kupitia burudani, mitandao ya kijamii, michezo, au njia za kisanaa kama muziki, maonyesho, matangazo, na kazi za kidijitali. Kwa mfano, mtu anaweza kuandika mashairi, tamthilia, au sinema zinazoingiza mapato, au kuunda maudhui yanayovutia wafuasi kwenye mitandao ya kijamii na hivyo kupata kipato. Vilevile, taaluma zinazohusiana na michezo na sanaa zinaweza kutoa fursa za kazi kwa kutumia lugha kwa ufanisi. Kwa hivyo, ubidhaishaji wa lugha si tu njia ya mawasiliano, bali pia ni chombo cha kiuchumi kinachowezesha kukuza vipaji vya ubunifu, mawasiliano, na kuunda mapato katika nyanja mbalimbali. Mtaala na Muhtasari wa mitaala inaonesha fursa hii kama ilivyowasilishwa katika Jedwali Na. 7.

Jedwali Na. 6: Malengo ya Somo la Kiswahili (Kidato cha V-VI)

Somo	Kipengele	Lengo mahsusi
Kiswahili	Malengo ya Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI	Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake

Chanzo: Muhtasari wa Kiswahili Elimu ya Sekondari Kidato cha V-VI (2023, uk. 2)

Jedwali Na. 7 linaonesha kuwa mojawapo ya malengo mahsusi ya somo la Kiswahili kwa Kidato cha V-VI ni kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha mwanafunzi kujiajiri, kuajiriwa na kuyamudu maisha kwa kutumia vizuri mazingira yake. Hii inaonesha kuwa ufundishaji wa Kiswahili katika ngazi hii haujikusanyi tu kwenye umahiri wa lugha, bali pia unalenga katika ukuaji wa kijamii na kiuchumi wa mwanafunzi kupitia matumizi ya lugha katika maisha halisi na fursa za ajira. Kutokana na data, Kiswahili kinapata nafasi ya kipekee katika ujenzi wa uchumi kupitia uandishi wa vitabu, uandaaji wa maudhui ya kidijitali, tafsiri, na utoaji wa mafunzo kwa wageni, hivyo kuwa chombo cha uzalishaji wa kipato na fursa ya maisha bora kwa watumiaji wake. Pia, Kiswahili kinatambuliwa si tu kama chombo cha kielimu na kitamaduni, bali pia kama rasilimali ya kiuchumi.

Hii inalingana na Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ya Émile Durkheim, ambayo inaeleza kuwa kila kipengele cha jamii, kama elimu, dini, familia, lugha, uchumi na serikali, kina jukumu maalum katika kudumisha uthabiti, mshikamano, na maendeleo ya kijamii. Kwa mujibu wa data, somo la Kiswahili linalenga kuwajengea wanafunzi maarifa, ujuzi, na stadi zinazowawezesha kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia ipasavyo rasilimali na mazingira yanayowazunguka. Katika muktadha huu, elimu ya Kiswahili inatekeleza dhima ya kijamii kwa kuwaandaa wahitimu wenye uwezo wa kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Hivyo, somo la Kiswahili linachangia kuimarisha mawasiliano, mshikamano, uzalishaji, na maendeleo ya kijamii na kiuchumi, jambo linalodhihirisha kuwa mtaala mpya umezingatia misingi ya uamilifu wa kijamii inayosisitiza mchango wa elimu katika ustawi wa jamii.

Kama mtafiti, ninaona data hizi zinaonesha fursa kubwa kwa Vyuo Vikuu vinavyofundisha Kiswahili. Ubidhishaji wa lugha unaleta Kiswahili karibu na jamii kwa kuifanya iwe rahisi kueleweka, kuvutia, na kufikika kupitia burudani, mitandao, michezo, na njia za kisanaa, jambo linaloongeza mvuto wa kujifunza na kutumia lugha hiyo. Hii ni fursa kwa Vyuo Vikuu kwani inawawezesha kuendeleza tafsiri za kisayansi, teknolojia, biashara, na mawasiliano ya kimataifa kwa Kiswahili, ikichangia kuongeza ajira na kipato kwa wahitimu wanaotoa huduma za kitaalamu za lugha. Hata hivyo, changamoto ni kudumisha ubunifu huu kitaifa na kimataifa kutokana na ukosefu wa vifaa vya kisasa, mafunzo ya walimu, na mitazamo hasi ya kijamii kuhusu matumizi ya Kiswahili katika teknolojia na biashara. Hivyo, Vyuo Vikuu vinahitaji mikakati madhubuti kukuza na kuhimiza matumizi ya Kiswahili katika nyanja za kisayansi na ubunifu ili kuendeleza faida zake endelevu, ikiwemo ajira, kipato, na maendeleo.

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (154-165), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

4.6 Fursa za Kiswahili kama Lugha ya Kufundishia

Kwa mujibu wa Msanjila (2004) wanasema kuwa lugha ya kufundishia ni lugha inayotumika kufundishia masomo katika mfumo wa elimu wa nchi. Lugha ya kufundishia ni chombo muhimu kinachotumika kufikisha maarifa, ujuzi, na maadili darasani kati ya mwalimu na mwanafunzi. Kiswahili kama lugha ya kufundishia ni fursa kwa sababu inarahisisha ujifunzaji na kuimarisha uelewa wa wanafunzi, hususan wale wanaotumia Kiswahili kama lugha yao ya kwanza. Kwa kuzingatia data kutoka kwenye mtaala wa elimu ya sekondari, matumizi ya Kiswahili katika kufundisha yanaonesha kwamba wanafunzi wanaweza kuelewa dhana ngumu kwa urahisi zaidi, kushiriki darasani kwa nguvu zaidi, na kujifunza kwa ufanisi.

Hii fursa ya kutumia Kiswahili kama lugha ya kufundishia haiwezi kuhitimishwa tu kwa masuala ya kielimu; pia inafungua njia za ukuaji wa kipato, ajira, na uwezeshaji wa kijamii. Wanafunzi wenye umahiri wa Kiswahili wanapopewa nafasi ya kufanya tafsiri, uhariri, na huduma za lugha, wanaweza kupata kazi katika elimu, vyombo vya habari, utawala, biashara, na TEHAMA, hivyo kuongeza mchango wao wa kielimu na kiuchumi katika jamii. Ushahidi wa fursa hii unatokana na Sera ya Elimu na Mafunzo (Toleo la 2023) inayotambua Kiswahili kama lugha ya taifa na chombo kikuu cha kufundishia katika ngazi mbalimbali kama ilivyobainishwa hapa chini:

"*Hivi sasa, lugha za kufundishia nchini Tanzania ni Kiswahili na Kiingereza. Kiswahili hutumika kufundishia elimu ya awali na msingi na pia hufundishwa kama somo. Katika shule za sekondari, vyuo vya ualimu ngazi ya stashahada, vyuo vya ufundi, na vyuo vya elimu ya juu, Kiingereza hutumika kama lugha ya kufundishia huku Kiswahili kikiwa somo. Aidha, Kiswahili pia hutumika kama lugha ya kufundishia katika vyuo vya ualimu ngazi ya cheti, vyuo vya ufundi stadi, na baadhi ya shule za sekondari pale inapohitajika."* Sera ya Elimu na Mafunzo, 2023, uk. 57).

Data hizi zinaonesha kuwa Kiswahili kama lugha ya kufundishia ni chombo muhimu cha kufikisha maarifa, ujuzi na maadili kwa wanafunzi. Kwa kutumia Kiswahili, hasa kwa wale wanaotumia lugha hiyo kama ya pili, ujifunzaji unarahisishwa na ushiriki darasani unazidi kuimarika. Hoja hii inashihirisha dhamira ya serikali ya kuimarisha nafasi ya Kiswahili kama lugha kuu ya kufundishia nchini Tanzania. Kupitia Kiswahili, sera inalenga kukuza uelewa wa pamoja, usawa wa fursa za kielimu, na kuendeleza utambulisho wa kitaifa. Wakati huohuo, sera hii mpya inatambua umuhimu wa lugha za kimataifa kama Kiingereza katika mazingira maalumu ya kielimu, hivyo kuleta uwiano kati ya ukuzaji wa Kiswahili na ushirikiano wa kimataifa.

Kwa mujibu wa Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ya Émile Durkheim, kila kipengele cha jamii, ikiwemo lugha, kina jukumu muhimu katika kudumisha mshikamano, utulivu, na maendeleo ya kijamii. Data zinaonesha kuwa matumizi ya Kiswahili kama lugha ya kufundishia yanakuza mawasiliano yenye ufanisi, huongeza ushiriki wa wanafunzi katika mchakato wa ujifunzaji, na huchangia usawa wa kijamii kwa kuwapa fursa sawa za upatikanaji wa maarifa. Aidha, matumizi ya Kiswahili yanafungua fursa mbalimbali za ajira katika nyanja za tafsiri, ukalimani, uhariri, uandishi, na mawasiliano. Hivyo, Kiswahili si tu nyenzo ya kufundishia na kujifunzia, bali pia ni chombo muhimu cha kijamii kinachokuza mshikamano wa kitaifa, ustawi wa jamii, na maendeleo endelevu ya taifa, jambo linaloendana na dhana ya Durkheim kuhusu mchango wa taasisi za kijamii katika kuimarisha uamilifu wa jamii.

Kutokana na data zilizotolewa, ufundishaji wa Kiswahili ni fursa muhimu kiuchumi na kielimu kwa vyuo vinavyofundisha lugha hii, kwani unawawezesha wanafunzi kupata ujuzi unaoweza kuwaletea ajira na kipato katika nyanja mbalimbali za elimu, utawala, media, na biashara. Lugha hii inarahisisha ufikishaji wa maarifa, ujuzi, na maadili darasani, hususani kwa wanafunzi wanaotumia Kiswahili kama lugha yao ya kwanza, jambo linaloongeza uelewa na ushiriki darasani. Sera mpya ya elimu na mafunzo inathibitisha dhamira ya serikali ya kuimarisha Kiswahili kama chombo kikuu cha kufundishia, ikilenga kuibua fursa za kiuchumi kwa wanafunzi huku ikikuza uelewa wa pamoja na utambulisho wa kitaifa.

4.7 Fursa ya Kiswahili Kama Nyenzo ya Mawasiliano Kimataifa

Kwa mujibu wa Osore (2018), nyenzo ya mawasiliano kimataifa inamaanisha uwezo wa lugha kutumika kuunganisha watu wa mataifa mbalimbali katika nyanja za kidiplomasia, biashara, elimu, teknolojia na utamaduni. Kwa maneno mengine, nyenzo ya mawasiliano kimataifa ni lugha au chombo kinachotumika kuwezesha mawasiliano kati ya watu kutoka mataifa na tamaduni tofauti, hivyo kurahisisha ubadilishanaji wa maarifa, biashara, elimu, na diplomasia. Kwa upande wa Kiswahili, lugha hii inachukuliwa kama nyenzo ya mawasiliano kimataifa kwa sababu inatumika si tu katika nchi nyingi za Afrika Mashariki na Kati, bali pia inaeneza uwepo wake katika mazingira ya elimu, biashara, na diplomasia duniani, ikiwemo mchakato wa tafsiri, uwasilishaji wa taarifa, na mawasiliano ya kitaalamu.

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (154-165), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

Hii inatoa fursa kubwa kwa wataalamu wa Kiswahili, kwani inawapa uwezo wa kupata ajira na kushiriki katika nyanja mbalimbali kama elimu, tafsiri, utawala, vyombo vya habari, biashara, na TEHAMA. Aidha, kuendeleza Kiswahili kama lugha ya mawasiliano kimataifa kunachangia ukuaji wa taaluma na uwekezaji wa kiuchumi, huku pia likiwa chanzo cha maendeleo binafsi, ikiwa ni pamoja na kupata kipato, kujiajiri, na kushiriki katika miradi ya kimataifa inayohitaji ujuzi wa Kiswahili. Kiswahili kinaonekana kuwa nyenzo ya fursa kwa sababu kinaweza kutumika kama kipengele cha ajira na biashara, kikiwezesha wataalamu na wahitimu kuongeza mapato yao, kujenga biashara zao, na kushiriki kikamilifu katika miradi ya kitaalamu na kimataifa. Data zinazoonesha hili zinaonesha kuwa matumizi ya Kiswahili katika elimu, biashara, na diplomasia vinaongeza thamani yake kama chombo cha mawasiliano kimataifa, na hivyo kuifanya kuwa fursa halisi ya kiuchumi na kitaaluma kwa wahitimu na wataalamu wa lugha. Sera ya Elimu na Mafunzo (Toleo la 2023) inatambua Kiswahili kuwa lugha yenye hadhi ya kikanda na kimataifa, kama inavyosema,

"*Lugha hii [Kiswahili] pia imekua kwa kiwango cha kimataifa, na hutumika na watu wengi kupata maarifa na ujuzi katika nyanja na ngazi mbalimbali za elimu. Aidha, Tanzania imeridhia itifaki za Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kuhusiana na maendeleo na matumizi ya Kiswahili, ambapo Tanzania imechaguliwa kuwa makao makuu ya Taasisi ya Kuendeleza Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.*" (Sera ya Elimu 2023, Kifungu 3.9, uk. 55)

Kifungu hiki kinaonesha kuwa serikali ya Tanzania imechukua jukumu la kimkakati la kukuza Kiswahili ndani na nje ya mipaka yake, jambo linaloliweka taifa katika nafasi ya kipekee kama kitovu cha usambazaji wa maarifa ya Kiswahili barani Afrika. Hali hii inapanua wigo wa Kiswahili kutoka ngazi ya kitaifa hadi kimataifa, na kuifanya lugha hii kuwa chombo cha diplomasia, biashara, elimu, na utamaduni wa pamoja wa Afrika Mashariki. Hii inaendana na utafiti wa Ojwang (2008) unaodai kuwa kukuza lugha kwa kiwango cha kikanda huimarisha uhusiano wa kiutamaduni, kielimu, na kiuchumi kwa kuwezesha mawasiliano na uelewano wa pamoja miongoni mwa mataifa.

Hoja hii inahusiana na Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ya Émile Durkheim kwa kuwa inaonesha jinsi lugha ya Kiswahili inavyotekeleza majukumu muhimu katika kudumisha umoja, utulivu, na mshikamano wa kijamii. Kwa mujibu wa nadharia hii, kila kipengele cha jamii, ikiwemo lugha, kina dhima maalumu inayochangia ufanisi na uthabiti wa mfumo mzima wa kijamii. Katika muktadha huu, kutambuliwa kwa Kiswahili kama lugha ya kikanda na kimataifa kunaimarisha nafasi yake kama chombo cha mawasiliano, elimu, na utambulisho wa kitaifa. Aidha, hadhi hii hupanua matumizi ya Kiswahili katika nyanja mbalimbali za kijamii, kiuchumi, na kitaaluma, hivyo kuchangia ushirikiano wa kijamii na maendeleo ya jamii kwa ujumla. Hivyo, hoja hii inadhihirisha kwamba Kiswahili kinaendelea kutekeleza jukumu lake la kiuamilifu katika kuimarisha mshikamano na maendeleo ya taifa ndani na nje ya mipaka yake.

Kama mtafiti, naona data hizi zinathibitisha kuwa Kiswahili lina fursa kubwa kama nyenzo ya mawasiliano kimataifa, jambo linaloweza kufaidisha Vyuo Vikuu vinavyofundisha Kiswahili. Kutambua Kiswahili kuwa lugha yenye hadhi ya kikanda na kimataifa kunawawezesha vyuo kutoa elimu inayojenga ujuzi wa kimataifa, kukuza tafsiri, utafiti, na diplomasia ya lugha, na hivyo kuongeza umaarufu na mchango wa taaluma za Kiswahili katika nyanja za kielimu, kisiasa, na kiuchumi. Hii ni fursa muhimu kwani inapanua wigo wa masomo ya Kiswahili, inawapa wanafunzi na walimu nafasi ya kushiriki katika mazungumzo ya kimataifa, na kuimarisha uhusiano wa kiutamaduni na kielimu barani Afrika.

Hata hivyo, changamoto kubwa inaweza kuwa upungufu wa rasilimali, miundombinu, na mafunzo maalum kwa walimu na wanafunzi ili kuendana na viwango vya kimataifa, sambamba na ushindani kutoka kwa lugha nyingine za kimataifa kama Kiingereza na Kifaransa, ambazo zinatawala katika biashara na elimu ya juu. Kwa hiyo, licha ya uwepo wa fursa pana kupitia TEHAMA, bado kuna haja ya kuwepo kwa sera madhubuti, uwekezaji wa kifedha, na juhudi za kitaalamu ili kuimarisha uwezo wa Kiswahili kutumika kikamilifu kama nyenzo ya mawasiliano, elimu, na maendeleo katika ngazi ya kimataifa.

4.8 Fursa ya Kutumia TEHAMA

Kwa mujibu wa TATAKI (2019: 627), TEHAMA ni kifupisho cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. TEHAMA inamaanisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika kukusanya, kuhifadhi, kuchakata, kusambaza, na kubadilishana taarifa kwa njia ya kielektroniki. Inahusisha vifaa na mifumo kama kompyuta, simu janja, mtandao (*internet*), programu, na mitandao ya kijamii vinavyorahisisha mawasiliano, upatikanaji wa taarifa, na utoaji wa huduma kwa ufanisi katika nyanja mbalimbali kama elimu, biashara, afya na utawala.

ISSN 2348-3156 (Print)
International Journal of Social Science and Humanities Research ISSN 2348-3164 (online)
Vol. 14, Issue 4, pp: (154-165), Month: October - December 2026, Available at: www.researchpublish.com

Fursa kubwa katika mwelekeo huu mpya ni TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano). TEHAMA inawawezesha wanafunzi kutumia zana za kidijitali kama video, kompyuta, na programu za mtandao kutafsiri na kukalimani kwa ufanisi, kuhariri maandiko, na kufanikisha mawasiliano ya lugha kwa kiwango kikubwa. Hii inazalisha fursa za maisha halisi, ikiwemo kupata kipato kupitia huduma za tafsiri na ukalimani, kujiajiri katika nyanja za elimu, sanaa, mitandao, na biashara, na kuendeleza taaluma ya Kiswahili kuwa na thamani kiuchumi na kijamii. Jedwali Na. 7 linadokeza matumizi ya mbinu za kiteknolojia (TEHAMA) katika ufundishaji wa Kiswahili, ikiwemo video, kompyuta, na zana nyingine za kidijitali, zikilenga kuboresha mbinu za kufundisha na kujifunza. Zingatia Jedwali Na. 8.

Jedwali Na. 7: Umahiri wa Kutumia TEHAMA

Somo	Umahiri Mkuu	Umahiri Mahususi
Kiswahili	Kutumia TEHAMA kutangaza kazi za sanaa sanifu	׀ Kutumia TEHAMA kutangaza kazi za sanaa sanifu

Chanzo: Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V - VI (2023, uk. 37)

Jedwali Na. 8 linaonesha kwamba umahiri mkuu na mahususi unalenga kutumia TEHAMA katika kutangaza na kuendeleza kazi za sanaa sanifu, kama ilivyobainishwa katika Mtaala wa Elimu ya Sekondari Kidato cha V–VI. Fursa hii inalingana na Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ya Émile Durkheim kwa kuwa TEHAMA huchangia kuimarisha mawasiliano, upatikanaji wa taarifa, usambazaji wa maarifa, na ushirikiano miongoni mwa wanajamii. Kupitia matumizi ya zana za kidijitali kama kompyuta, video, mitandao ya kijamii, na programu mbalimbali, wanafunzi wanaweza kukuza umahiri wa uandishi, uhariri, ubunifu, na utangazaji wa kazi za sanaa sanifu kwa ufanisi zaidi. Hali hii huongeza ushiriki wa kijamii, huimarisha mwingiliano wa kielimu na kitaaluma, na hupanua fursa za kiuchumi zinazotokana na kazi za ubunifu. Hivyo, matumizi ya TEHAMA katika sanaa sanifu yanatekeleza dhima ya kijamii ya kuimarisha mshikamano, maendeleo, na ustawi wa jamii, jambo linalosisitizwa na Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii.

Fursa ya kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili ni muhimu kwa Vyuo Vikuu vinavyotoa programu za Kiswahili. Matumizi ya zana za kidijitali kama kompyuta, video, majukwaa ya mtandaoni na programu mbalimbali hurahisisha upatikanaji wa taarifa, usambazaji wa maarifa, na uboreshaji wa umahiri wa wanafunzi katika uandishi, uhariri, tafsiri, na sanaa za maonyesho. Hali hii huifanya lugha ya Kiswahili kuwa rahisi kufikika, yenye mvuto, na inayoendana na maendeleo ya teknolojia ya kisasa. Kwa mujibu wa Nadharia ya Uamilifu wa Kijamii ya Émile Durkheim, TEHAMA huchangia kuimarisha mawasiliano, ushirikiano, na mshikamano wa kijamii kwa kuwezesha mwingiliano wa kielimu na kitaaluma miongoni mwa walimu, wanafunzi, na wadau wengine. Hivyo, matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili si tu yanaboresha ubora wa elimu, bali pia yanachangia maendeleo ya kijamii na kiuchumi kwa kuandaa wahitimu wenye ujuzi unaokidhi mahitaji ya jamii ya kidijitali.

Hata hivyo, changamoto zinaweza kujitokeza pale ambapo Vyuo Vikuu havina miundombinu ya TEHAMA iliyoimarishwa au pale ambapo walimu hawana ujuzi wa kutosha wa kutumia teknolojia hizo kwa ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji. Hali hii inaweza kupunguza kwa kiasi kikubwa manufaa yanayotarajiwa ya matumizi ya TEHAMA katika kukuza na kufundisha Kiswahili. Aidha, ukosefu wa vifaa vya kisasa, mtandao hafifu na mafunzo duni ya kitaalamu unaweza kuathiri utekelezaji wa mbinu bunifu za ufundishaji. Kwa hivyo, ingawa fursa ya matumizi ya TEHAMA ni halisi na ina mchango mkubwa katika maendeleo ya elimu ya Kiswahili, inahitaji uwekaji wa mikakati madhubuti ya kuboresha miundombinu, kuongeza mafunzo ya walimu na kuhakikisha upatikanaji endelevu wa zana za kidijitali.

5. HITIMISHO

Makala haya yameainisha fursa za lugha ya Kiswahili zilizopo kwenye mitaala ya Kiswahili kufuatia utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 (Toleo la 2023) nchini Tanzania. Uchambuzi wa maandiko unaonesha kuwepo Kwa fursa nane za kiuchumi na kitaaluma zilizojitokeza katika Sera na Mtaala Mpya wa Elimu nchini Tanzania. Matokeo yanaonesha kuwa vyuo vikuu vimeanza kuoanisha mitaala yake na mwelekeo wa sera kwa kuanzisha programu na kozi mpya zinazohusiana na kujiari, kupata kipato na kuendeleza taaluma kupitia Kiswahili fursa hizo ni tafsiri na ukalimani, uhariri na uandishi, ubidhaishaji wa lugha, ubunifu wa lugha, Sanaa na uigizaji, Kiswahili kama lugha ya kufundishia, ubunifu katika ufundi wa lugha na matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA). Ni wazi kuwa mafanikio ya fursa hizi yanategemea uwekezaji wa makusudi katika uandaaji wa walimu mahiri, upatikanaji wa vifaa vya kujifunzia, na utafiti endelevu. Hatua hizi zitahakikisha Kiswahili kinabaki kuwa nguzo imara ya maendeleo ya kijamii, kiuchumi, na kiutamaduni kwa Taifa.

MAREJEO

[1] Adolph, E. (2023). Fursa zitokanazo na makongamano ya vyama vya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania [Makala ya kongamano isiyochapishwa]. Kongamano la Nane la Kimataifa la CHAUKIDU, MS Training Centre for Development Cooperation (MSTCDC), Arusha, Tanzania.

[2] Durkheim, E. (1912). The division of labour in society. Alcan.

[3] Durkheim, E. (1984). The division of labour in society. Macmillan. (Kazi ya awali ilichapishwa mwaka 1893).

[4] Maganga, C. (2008). Juhudi za ukuzaji wa Kiswahili Tanzania Bara. Katika J. G. Kiango (Mh.), Ukuzaji wa istilahi za Kiswahili. TUKI.

[5] Mbaabu, I. (2007). Historia ya usanifishaji wa Kiswahili. TUKI.

[6] Matei, A. (2008). Fani ya fasihi simulizi kwa shule za upili. Jomo Kenyatta Foundation.

[7] Mazrui, A., & Mazrui, A. (1998). The power of Babel: Language and governance in the African experience. University of Chicago Press.

[8] Mazrui, A. M., & Shariff, I. N. (1994). The Swahili: Idiom and identity of an African people. Africa World Press.

[9] Mlaga, W. (2021). Ufundishaji na ujifunzaji katika nyuga za kiinsia: Habari iliyopo inakabiliwa? Jarida la Mnyampala, 2(1), 106–119.

[10] Msanjila, Y. P. (2004). Kiswahili kitumike kufundishia sekondari na elimu ya juu Tanzania. TUKI.

[11] Mutembei, A. (2011). Kukitandawazisha Kiswahili kupitia simu za kiganjani: Tafakari kuhusu isimujamii. Swahili Forum, 18, 198–210.

[12] Ojwang, B. (2008). Prospects of Kiswahili as a regional language in a socioculturally heterogeneous East Africa. Journal of International and Intercultural Communication, 1(4), 327–347.